

JIFUNZE KICHINA



每日汉语

斯瓦希里语 05



国家汉办/孔子学院总部
Hanban/Confucius Institute Headquarters



中国国际广播电台
CHINA RADIO INTERNATIONAL

中国国际广播出版社

05

JIFUNZE KICHINA

每日汉语

中国国际广播出版社



目录 / Yaliyomo

第四十八课 在药店

Somo la 48 Katika duka la dawa 1

第四十九课 急诊

Somo la 49 Matibabu ya dharura 7

第五十课 交费取药

Somo la 50 Kutoa malipo na kuchukua dawa 12

第五十一课 探病

Somo la 51 Kutembelea mgonjwa 18

第五十二课 幼儿园

Somo la 52 Shule ya chekechea 24

第五十三课 大学

Somo la 53 Chuo kikuu 30

第五十四课 在图书馆

Somo la 54 Katika Maktaba 36



目录 / Yaliyomo

第五十五课 与同学聊天

Somo la 55 Maongezi kati ya wanafunzi 42

第五十六课 谈论网吧

Somo la 56 Baa ya kutembea mtandao
wa internet 48

第五十七课 报名


Somo la 57 Kujiandikisha 54

第五十八课 在酒吧

Somo la 58 Katika baa 60

第四十八课 在药店

Somo la 48 Katika duka la dawa



A: Kwanza tunarudia maneno tuliyojifunza kwenye somo la 47:

Wǒ gěi nǐ kāi diǎn er gǎn mào yào.

1. 我给你开点儿感冒药。Nakuandikia dawa za mafua.

Měi tiān chī jǐ cì?

2. 每天吃几次? Natakiwa kula mara ngapi kwa siku?

Yì tiān sān cì, měi cì yí piàn.

3. 一天三次, 每次一片。Mara tatu kwa siku, kila mara kidonge kimoja.

Huí qù duō hē shuǐ, hǎo hǎo xiū xi.

4. 回去多喝水, 好好休息。Unywe maji mengi na kupumzika vizuri baada ya kurudi nyumbani.

A: Sasa tuanze somo la 48:



今日关键 Maneno mapya ya leo

Zuì jìn wǒ yá téng.

1. 最近我牙疼。Siku hizi nahisi maumivu kwenye meno.

Yīng gāi chī shén me yào ne?

2. 应该吃什么药呢? Ningetumia dawa gani?

Zhè zhǒng yào xiào guǒ bú cuò.

3. 这种药效果不错。Dawa hii ina ufanisi mzuri.

Yǒu fù zuò yòng ma?

4. 有副作用吗? Dawa hii ina madhara?

A: Ukihisi maumivu kwenye meno, unaweza kumwambia daktari kuwa, 最近我牙疼。Siku hizi nahisi maumivu kwenye meno.

B: 最近我牙疼。Matamshi yake kwa herufi za kiswahili ni: **zui jin wo ya teng**

A: 最近 **zui jin**, siku hizi, 我 **wo**, mimi, 牙 **ya**, meno, 疼 **teng**, uma,

B: 最近我牙疼。 **zui jin wo ya teng**

对话一 Maongezi ya kawaida ya wachina (1)

A: 最近我牙疼。Siku hizi nahisi maumivu kwenye meno.

B: 最近我牙疼。 **zui jin wo ya teng**

A: 什么时候开始的? Hali hii ilianza lini? 什么时候 **she me shi hou**, lini, 开始的 **kai shi de**, anza.

B: 什么时候开始的? **shen me shi hou kai shi de**

A: 前天。Juzi.

B: 前天。 **qian tian**

A: Ukitaka kujua dawa gani inatibu ugonjwa wake, unaweza kumwuliza daktari kuwa, 应该吃什么药呢, ningetumia dawa gani?

B: 应该吃什么药呢? **ying gai chi shen me yao ne**

A: 应该 **ying gai**, takiwa, 吃 **chi**, kula, 什么 **shen me**, gani, 药 **yao**, dawa, 呢 **ne**, kisaidizi cha neno kwa kuuliza.

B: 应该吃什么药呢? **ying gai chi shen me yao ne**

对话二 Maongezi ya kawaida ya wachina (2)

A: 应该吃什么药呢? Ningetumia dawa gani?

B: 应该吃什么药呢? **ying gai chi shen me yao ne**

A: 你试试这种药。Jaribu dawa ya aina hii. 你 **ni**, wewe, 试试 **shi shi**, jaribu, 这种 **zhe zhong**, aina hii, 药 **yao**, dawa.

B: 你试试这种药。 **ni shi shi zhe zhong yao**

A: 行。Sawa.

B: 行。 **xing**

A: Daktari anapendekeza mgonjwa wake atumie dawa ya aina fulani kwa kusema, 这种药效果不错, ufanisi wa dawa ya aina hii ni mzuri.

B: 这种药效果不错。 **zhe zhong yao xiao guo bu cuo**

A: 这种 **zhe zhong**, aina hii, 药 **yao**, dawa, 效果 **xiao guo**, ufanisi, 不错 **bu cuo**, mzuri.

B: 这种药效果不错。 **zhe zhong yao xiao guo bu cuo**

A: 有副作用吗? Dawa hii ina madhara mengine?

B: 有副作用吗? **you fu zuo yong ma**

A: 有 **you**, kuna, 副作用 **fu zuo yong**, madhara, 吗 **ma**,
kisaidizi cha neno kwa kuuliza.

对话三 Maongezi ya kawaida ya wachina (3)

A: 这种药效果不错。 Ufanisi wa dawa ya aina hii ni mzuri.

B: 这种药效果不错。 **zhe zhong yao xiao guo bu cuo**

A: 有副作用吗? Dawa hii ina madhara mengine?

B: 有副作用吗? **you fu zuo yong ma**

A: 没什么副作用。 Haina madhara. 没 **mei**, haina, 什么 **shen me**, yoyote.

B: 没什么副作用。 **mei shen me fu zuo yong**



Vidokezo vya utamaduni


Katika elimu ya matibabu ya kichina, wagonjwa wanapotibiwa pia wanaweza kushughulikia hali ya miili yao, kuongeza uwezo wa kinga, kwa kufanya hivyo hawawezi kupata madhara makubwa, hivyo wagonjwa wengi waliopatwa na ugonjwa sugu, au wazee na watoto wanapotibiwa, huwa wanaweza kuchagua kwanza matibabu ya kichina. Katika maduka ya dawa za mitishamba ya kichina, kuna dawa za aina mbalimbali,

wahudumu wanaweza kuwasaidia wateja kupata dawa walizoandikiwa na madaktari, ambapo wateja pia wanaweza kuwaambia wahudumu hali yao ya ugonjwa, ili wawasaidie kupata dawa zinazowafaa.



第四十九课 急诊

Somo la 49 Matibabu ya dharura



A: Kwanza tunarudia maneno tuliyojifunza kwenye somo la 48:

Zuì jìn wǒ yá téng.

1. 最近我牙疼。Siku hizi nahisi maumivu kwenye meno.

Yīng gāi chī shén me yào ne?

2. 应该吃什么药呢? Ningetumia dawa gani?

Zhè zhǒng yào xiào guǒ bú cuò.

3. 这种药效果不错。Dawa hii ina ufanisi mzuri.

Yǒu fù zuò yòng ma?

4. 有副作用吗? Dawa hii ina madhara?

A: Sasa tuanze somo la 49:



今日关键 Maneno mapya ya leo

Kuài jiào jiù hù chē!

1. 快叫救护车! Piga haraka simu ya kuomba gari la huduma ya kwanza.

Tā liú le hěn duō xiě.

2. 他流了很多血。Ametokwa na damu nyingi.

Méi yǒu shēng mìng wēi xiǎn ba?

3. 没有生命危险吧? Hana hatari ya maisha?

Zuì hǎo zhù yuàn guān chá jǐ tiān.

4. 最好住院观察几天。Bora alazwe hospitali kwa siku kadhaa ili tuangalie.

A: Ukiona mtu fulani amejeruhiwa, unaweza kuwaambia watu wengine kuwa, 快叫救护车! Piga haraka simu ya kuomba gari la huduma ya kwanza!

B: 快叫救护车! Matamshi yake kwa herufi za kiswahili ni: **kuai jiao jiu hu che**

A: 快 **kuai**, haraka, 叫 **jiao**, omba, 救护车 **jiu hu che**, gari la huduma ya kwanza.

B: 快叫救护车! **kuai jiao jiu hu che**

对话一 Maongezi ya kawaida ya wachina (1)

A: 有人受伤了! Kuna mtu aliyejeruhiwa! 有 **you**, kuna, 人 **ren**, mtu, 受伤了 **shou shang le**, jeruhiwa.

B: 有人受伤了! **you ren shou shang le**

A: 快叫救护车! Piga haraka simu ya kuomba gari la huduma ya kwanza!

B: 快叫救护车! **kuai jiao jiu hu che**

A: 他流了很多血。Ametokwa na damu nyingi.

B: 他流了很多血。 **ta liu le hen duo xie**

A: 他 **ta**, yeye, 流 **liu**, tokwa, 了 **le**, kisaidizi cha neno, 很多 **hen duo**, nyingi, 血 **xie**, damu.

对话二 Maongezi ya kawaida ya wachina (2)

A: 他流了很多血。Ametokwa na damu nyingi.

B: 他流了很多血。 **ta liu le hen duo xie**

A: 快叫救护车! Piga haraka simu ya gari la kutoa huduma ya kwanza!

B: 快叫救护车! **kuai jiao jiu hu che**

A: Mtu fulani akijeruhiwa vibaya, unaweza kumwuliza daktari kuwa, 没有生命危险吧, hana hatari ya maisha?

B: 没有生命危险吧? **mei you sheng ming wei xian ba**

A: 没有 **mei you**, hakuna, 生命 **sheng ming**, maisha, 危险 **wei xian**, hatari, 吧 **ba**, kisaidizi cha neno.

B: 没有生命危险吧? **mei you sheng ming wei xian ba**

A: 不要紧。最好住院观察几天。Si mbaya sana, bora alazwe hospitali siku kadhaa ili tuangalie.

B: 不要紧。最好住院观察几天。 **bu yao jin. zui hao zhu yuan guan cha ji tian**

A: 不要紧 **bu yao jin**, si mbaya, 最好 **zui hao**, bora, 住院 **zhu yuan**, lazwa hospitali, 观察 **guan cha**, angalia, 几天 **ji tian**, siku kadhaa.

对话三 Maongezi ya kawaida ya wachina (3)

A: 没有生命危险吧? Hana hatari ya maisha?

B: 没有生命危险吧? **mei you sheng ming wei xian ba**

A: 不要紧。最好住院观察几天。Si mbaya sana, bora alazwe hospitali siku kadhaa ili tuangalie.

B: 不要紧。最好住院观察几天。**bu yao jin. zui hao zhu yuan guan cha ji tian**




Vidokezo vya utamaduni

Baadhi ya watu wanaona matibabu ya kichina hupata ufanisi pole pole, hivyo matibabu hayo yanafaa zaidi kutibu ugonjwa sugu. Hali halisi ni kuwa, matibabu ya kichina yanaonesha pia umuhimu wake wakati wa kutoa huduma ya kwanza kwa wagonjwa. Katika vitabu maarufu vilivyochapishwa katika zama za kale nchini China, mbinu za kutoa huduma ya kwanza kwa wagonjwa ni za aina mbalimbali kama vile kudunga sindano ya akyupancha, kufanya usingaji wa mwili, kushughulikia vizuri hali ya mifupa na kadhalika.

第五十课 交费取药

Somo la 50 Kutoa malipo na kuchukua dawa



A: Kwanza tunarudia maneno tuliyojifunza kwenye somo la 49:

Kuài jiào jiù hù chē!

1. 快叫救护车! Piga haraka simu ya kuomba gari la huduma ya kwanza.

Tā liú le hěn duō xiě.

2. 他流了很多血。Ametokwa na damu nyingi.

Méi yǒu shēng mìng wēi xiǎn ba?

3. 没有生命危险吧? Hana hatari ya maisha?

Zuì hǎo zhù yuàn guān chá jǐ tiān.

4. 最好住院观察几天。Bora alazwe hospitali kwa siku kadhaa ili tuangalie.

A: Sasa tuanze somo la 50:



今日关键 Maneno mapya ya leo

Qǐng nín xiān qù jiāo fèi.

1. 请您先去交费。Tafadhali kwanza nenda kutoa malipo.

Dài fu, qǔ yào.

2. 大夫, 取药。Daktari, nachukua dawa.

Zhè yì píng shì wài yòng de.

3. 这一瓶是外用的。Dawa ya chupa hii ni ya kupaka.